

Maswali

1. Eliya alimtii nani?
2. Ni nini ilikuwa adhabu kwa Waisraeli?
3. Mbona adhabu ilikuwako?
4. Eliya alienda wapi kwanza?
5. Eliya alilishwa na nani?
6. Alikuwa na chakula gani?
7. Baadaye Eliya alienda wapi?
8. Nani alimlinda huko?
9. Eliya alitaka afanyiwe nini?
10. Ni nini ilifanyika kwa chakula?
11. Nini ilifanyika kwa mtoto wa huyo mwanamke?
12. Tunajifunza nini kwa Eliya?

Majibu

1. Eliya alitii Bwana Mungu wa Israeli.
2. Adhabu kwa Waisraeli ni kutokuwa na mvua.
3. Kwa sababu Ahabu mfalme wa Israeli alikuwa muovu.
4. Eliya alienda kwa Kijito cha kerithi.
5. Alilishwa na Kunguru.
6. Alikuwa na mkate na nyama.
7. Alienda Sarepta.
8. Alilindwa na mwanamke mjane.
9. Alitaka yeye apewe chakula kwanza.
10. Chakula hakikuisha
11. Mtoto alikuwa mgonjwa na akafa.
12. Tunajifunza kumtii Mungu na kumuomba

SHULE YA JUMAPILI YA CBM



Awamu ya 1 Mwaka wa 1

27 Mungu analisha Eliya

Marejeo

1 Wafalme 17

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu anajali watumishi wake kila wakati


Maneno maalum

1. Eliya + asimama + amrisha
2. Ahabu + Mfalme + hakuna mvua + adhabu + ibada ya sanamu + Yezebeli
3. Ficha + kijito cha Kerithi + kunguru + chakula
4. Sarepta + mjane na mwanawe + chakula cha mwisho + kufa.
5. Eliya ale kwanza + unga + mafuta + kutoisha
6. Mtoto + mgonjwa + akafa + maombi + maisha mapya
7. Miaka tatu na nusu + mvua tena + Mungu anajali

27.1 Mtumishi Eliya alikuwa nabii wa Israeli. Mazungumzo yake ya kwanza yanatuonyesha kwamba alikuwa akisimama mbele ya Mungu wa Israeli na kusema mambo aliyokuwa akiamrishwa na Mungu.

27.2 Eliya aliambia Ahabu Mfalme wa Israeli kwamba, kwa mda mrefu hakutakuwa na mvua. Hii ilikuwa adhabu kwa maovu yote aliyoyafanya Ahabu. Alikuwa ameabudu miungu ya uongo na kuelegeza watu wake kufanya hivyo. Tena alikuwa na mke muovu aliyeitwa Yezebeli. Mungu akatuma Eliya na habari kwamba hakutakuwa na mvua Israeli.

27.3 Mungu alimwambia Eliya pahali atakakoenda kuchificha



kutoka kwa Mfalme. Ni lazima aende aishi karibu na kijito Kerithi. Anywe maji kutoka kwa kijito mpaka kikauke. Mungu alimletea chakula kwa njia isiyo ya kawaida. Kunguru walimwendea asubuhi na jioni. Walimlisha kwa

kumletea mkate na nyama. Baadaye kijito nacho kilikauka na kumfanya Eliya aame.

27.4 Mungu alimpeleka kwa mji wa Sarepta. Huu mji ulikuwa nje ya nchi ya Israeli. Ilikuwa salama kwa Eliya kutoroka Ahabu aliyekuwa akimtafuta kila wakati. Hapo Sarepta kulikuwa na mjane mwenye Mungu alimwambia amhudumie Eliya. Eliya alipofika mjini alimpata huyu mwanamke akiokota vijiti. Akamuuliza ampe maji anywe, akamletea maji na tena akamuuliza ampe chakula. Akamwambia kwamba alikuwa na chakula cha siku moja tu. Alikuwa ajitengenezee yeye na mtoto wake wale na wafe.



27.5 Huyu mwanamke hakukuwa Mwiisraeli lakini alijua kwamba Mungu ndiye alileta kiangazi na njaa. Eliya alimwambia amtengenezee chakula na ampe yeye ale kabla yao. Baadaye ale na

mtoto wakule. Eliya alimwakikishia kwamba hicho chakula hakitaisha. Huyu mwanamke alimuamini na akamuletea chakula.

Neno la Eliya lilikuwa kweli. Hakuishiwa na chakula kwa huo muda wote wa kiangazi. Pipa la unga na chupa ya mafuta vilikuwa vimejaa kila siku akienda kuchukuwa atengenezee chakula kingine. Tujue ni la maana na lazima tumueke Mungu mbele.



27.6 Walipokuwa wakiishi na Eliya, mtoto wa yule mwanamke alikuwa mgonjwa na akafa. Eliya alimpeleka huyo mtoto kwa chumba chake. Akaomba Mungu akirudia rudia. Mungu alimsikia na akamrudishia huyo kijana uzima.

27.7 Mungu aliendelea kulinda Eliya kwa miaka tatu na nusu mpaka mvua iliponyesha. Somo litakalofwata litakuwa juu ya vile mvua iliporudi Israel.

Mungu anatumia wakati wote hata kama maisha ni magumu.